**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI KILICHOKETI TAREHE 22/11/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO MANISPAA YA MTWARA MIKINDANI**

**WALIOHUDHURIA**

1. Mhe. Shadida A. Ndile - Mstahiki Meya - Mwenyekiti
2. Mhe. Saidi A. Nassoro - Naibu Meya - Mjumbe
3. Mhe. Masoud Dali - Diwani Naliendele - Mjumbe
4. Mhe. Ally A. Ally - Diwani Magengeni - Mjumbe
5. Mhe. Juma S. Ngeki - Diwani Jangwani - Mjumbe
6. Mhe. Lameck S. Mlaponi - Diwani Magomeni - Mjumbe
7. Mhe. Zuhura B. Mikidadi - Diwani V/Maalumu - Mjumbe
8. Mhe. Sixmund J. Lungu - Diwani Majengo - Mjumbe
9. COL Emanuel Mwaigobeko - Mkurugenzi - Katibu

**WATAALAM**

1. Ndg. Tamko M. Ally - Mkuu wa Idara ya Utumishi
2. Ndg. Juliana Manyama - Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
3. Dkt. Lusungu Mselela - K/Mkuu wa Idara ya Afya
4. Ndg. Hassan Kahungo - K/Mkuu wa Idara ya Mipango na Takwimu
5. Ndg. Ramadhani Marusu - Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
6. Ndg. Masumbuko Mtesigwa - Mkuu wa Idara ya Mazingira
7. Ndg. Mohamedi Longoi - Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika
8. Ndg. Tumaini Mosha - K/Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
9. Ndg. Hawa M. Mtima - K/Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
10. Ndg. Grayson A. Orcado - Mkuu wa Kitengo cha Sheria
11. Ndg. Flora Aloys - Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
12. Ndg. Acland Kambili - Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi
13. Ndg. Jamadi Omari - Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na Uhusiano
14. Ndg. Mariam M. Kimolo - Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipangomiji
15. Ndg. Alphonce Mulima - Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
16. Ndg. Helena Simbua - Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi
17. Eng. Sweetbert Mwajombe - K/Mkuu wa Idara ya Ujenzi
18. Ndg. Janeth J. Mhegelle - Afisa Biashara
19. Ndg. Eda S. Nalinga - Afisa Tawala
20. Ndg. Rukia A. Jaha - Mratibu wa Vikao

**WAALIKWA**

1. Ndg. Octavian S. Lyapembile - Afisa Tarafa Mikindani
2. Ndg. Saidi M. Kayangu - Afisa Tarafa Mtwara Mjini

**MUHT. NA. 143/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 04:40 asubuhi.

**MUHT. NA. 144/2022; KUTHIBITISHA AGENDA**

Katibu aliwasilisha agenda za kikao, wajumbe walizipitia na kuthibitisha.

**MUHT. NA. 145/2021: KUTHIBITISHA MUHTASARI**

Wajumbe walipitia muhtasari wa kikao cha tarehe 22/10/2021 kisha kuthibitisha kuwa kumbukumbu ya vikao vya Halmashauri.

**MUHT. NA. 146/2021: YATOKONAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI KILICHOFANYIKA TAREHE 22/10/2021**

| AZIMIO | UTEKELEZAJI WAKE |
|---|---|
| **MUHT. NA. 135/2021; Ufanyike uchunguzi wa fedha Tshs. Milioni 30 za Shule ya Sekondari Umoja**<br>Ufanyike ukaguzi wa matumizi ya Shilingi milioni 30 kwenye ukarabati wa maabara Shule ya Sekondari Umoja | Mkaguzi wa ndani ameanza kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha Tshs. 30,000,000 iliyotumika katika ukarabati wa maabara katika shule hiyo. |
| **Muht. Na. 140/2021; Mwalo wa milumba**<br>Ufanyike ufuatiliaji wa mwalo wa milumba kujua kama biashara ya samaki inafanyika usiku. | Utekelezaji umefanyika kwa kufanya doria. Pia kilifanyika kikao kilichohusisha Madiwani, Watendaji wa Kata, Watendaji wa Mitaa na Wenyeviti wa Mitaa wa Tarafa ya Mikindani siku ya tarehe 02/11/2021. |

Mjumbe alikieleza kikao kuwa, kufuatia hoja ya thamani ya matumizi ya fedha ya milioni 30 katika maabara ya Sekondari ya Umoja, Mkaguzi wa Ndani afanye Ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo za ukarabati wa jengo la maabara katika Sekondari ya Umoja.

Katibu alikieleza kikao kuwa kutokana na majukumu aliyonayo Mkaguzi wa ndani yamesababisha achelewe kuleta majibu, hivyo kikao kinachofuata majibu yatapatikana.

Mjumbe alishauri kikao kuwa mapendekezo ya kuuza samaki katika mwalo wa milumba kuanzia saa 11 alfajiri hadi saa 12 jioni ni mazuri, itasaidia kuwalinda wanawake. Hivyo mapendekezo haya yafanyiwe kazi.

Mjumbe alikieleza kikao kuwa, Halmashauri ina kazi ya kukusanya mapato, Viongozi wa Tarafa ya Mikindani waungane kuhakiki mapato yanapatikana.

**ILIAZIMIWA** kwamba; Watendaji waandikiwe barua za kuitisha mikutano ya wananchi ili kupeleka mapendekezo ya kuuza samaki katika mwalo wa milumba kuanzia saa 11 alfajiri hadi saa 12 jioni, Idara ya Uvuvi na Afisa Tarafa washiriki mikutano hiyo.

**MUHT. NA. 147/2021: TAARIFA YA FEDHA MWEZI OKTOBA 2021**

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara aliwasilisha taarifa ya fedha (Mapato na Matumizi) kwa mwezi Oktoba, 2021. Alikieleza kikao kuwa kwa Mwezi Oktoba Halmashauri imekusanya Tshs. 315,645,202.23 hivyo kuanzia Julai hadi Oktoba, 2021 Halmashauri imekusanya Tshs 1,040,879,153.90 sawa na asilimia 21% kati ya 33.2% zilizotakiwa kukusanya. Na Mapato ya ndani katika mfumo wa LGRCIS yalikuwa Tshs. 158,013,745.03 Mapato ya Ndani katika mfumo wa FFARS (Vituo vya kutolea huduma za Afya na Ada za Shule) ni Tshs.46,983,390.20 na Mapato ya Urasimishaji Ardhi ni Tshs 110,648,067.00. (ufukoni, Magomeni, Mitengo, na Shangani).

A. ALBAKI YA MWEZI SEPTEMBA 2021 NI TSHS. 654,033,526.99

B. MAPATO

| AINA YA MAPATO | MAPATO OKTOBA, 2021 |
|---|---:|
| Mapato ya ndani – LGRCIS NA FFARS | 315,645,202.23 |
| Ruzuku ya matumizi ya kawaida | 95,208,583.32 |
| Ruzuku ya Mishahara | 1,222,561,000.00 |
| Mifuko mbalimbali na Miradi | 1,181,846,478.33 |
| Posho ya Madiwani | 8,450,000.00 |
| **JUMLA NDOGO** | **2,823,711,263.88** |

C. MATUMIZI

| MAELEZO | MATUMIZI OKTOBA,2021 |
|---|---:|
| Jumla ya matumizi ya Miradi | 1,181,846,478.33 |
| Jumla kuu Matumizi Mapato ya Ndani | 396,530,695.18 |
| Jumal kuu ya Matumizi ya Ruzuku | 18,047,740.00 |
| Jumla kuu ya Matumizi ya Mishahara | 1,222,561,000.00 |
| Posho ya Madiwani | 8,450,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **2,827,435,913.51** |
| **Jumla Kuu ya Matumizi** | **2,827,435,913.51** |

Mjumbe alitaka kufahamu pango la nyumba na mabanda ukusanyaji wake wa aina gani.

Katibu alikieleza kikao kuwa kuna mabanda yamefungwa na mabanda mengine wamiliki wanalipa kidogo kidogo.

Mjumbe alikieleza kikao kuwa taarifa ya Fedha iainishe maeneo husika yanayokusanya mapato, kwa kutaja chanzo husika ili kuweza kuchukua hatua.

**ILIAZIMIWA** kwamba; Taarifa ya Fedha iainishe mapato kwenye masoko na stendi.

Katibu alikieleza kikao kuwa aliwahi kufuatilia kuhusu tozo ya ushuru wa huduma ya makaa ya mawe na kuambiwa wamelipia yanakotoka, lakini aliagiza wafuatilie huko yanakotoka ili kujiridhisha kama kweli yamelipiwa.

Mjumbe alikieleza kikao kuwa Halmashauri isilikalie kimya jambo hili kwa kuwa wananchi wanaathirika na vumbi lake, hivyo hoja ya Ushuru wa huduma za Mji ifuatiliwe kiundani.

Mkuu wa Idara ya mazingira alikieleza kikao kuwa Timu ya NEMC iliwahi kwenda na kusitisha shughuli ya upakiaji na yalitolewa maelekezo ya namna bora ya kuhifadhi, hivyo Idara itaendelea kufuatilia kuona kama maagizo ya NEMC yanafanyiwa kazi.

Mjumbe alikieleza kikao kuwa eneo la machinjio na mapato yatokanayo na samaki yaangaliwe upya, alishauri eneo hili litolewe macho ili kuwezesha kupatikana mapato.

Kaimu Mkuu Idara ya Mifugo na Uvuvi alikieleza kikao kuwa mapato yatokanayo na samaki yamepungua kwa sababu gharama ya leseni ya uvuvi kwa Manispaa ni kubwa ukilinganisha na Halmashauri ya Wilaya Mtwara, hivyo wavuvi wanakata leseni Halmashauri ya Wilaya Mtwara. Pia mapato ya samaki waliokuwa wanatoka Msumbiji yamepungua kwa sasa kwa kuwa kuna kituo kimoja tu cha kushushia samaki ambacho kipo Halmashauri ya Wilaya Mtwara.

Mjumbe alikieleza kikao kuwa vibali vya sherehe viangaliwe hasa kipindi hiki, kwa kuwa mapato ni madogo na yanavuja sana eneo hili.

Katibu alikieleza kikao kuwa Waheshimiwa Madiwani waliopo katika maeneo yao waisaidie Halmashauri kwa kuangalia kama wahusika wanavibali.

Mjumbe alikieleza kikao kuwa vibali vya sherehe ilipitishwa kuwa ni Tshs. 50,000 kama kuna mabadiliko yawekwe wazi kwa kuwa vibali vinavyotolewa sasa gharama inaonesha ni chini ya kiasi hicho.

Katibu alikieleza kikao kuwa hakuna mabadiliko ya gharama ya vibali vya sherehe.

**ILIAZIMIWA** kwamba; Afisa aliyetoa kibali kwa gharama pungufu alipe gharama za kibali alizopunguza na risiti ionekane kikao kijacho.

Mjumbe alikieleza kikao kuwa kila mtu aongeze nguvu katika eneo lake ili kukusanya mapato.

**ILIAZIMIWA** kwamba; Kila chanzo cha mapato kiwe na mkusanya mapato ili kudhibiti mapato kupotea.

**MUHT. NA. 148/2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UJENZI WA MADARASA 22 KUPITIA FEDHA ZA UVIKO 19**

Afisa Mipango alikieleza kikao kuwa Serikali imepata mkopo wenye masharti nafuu wa Dola za Kimarekani milioni 567 sawa na Shilingi trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha la kimataifa IMF kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19. Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani ilipokea fedha kiasi cha shilingi milioni mia nne na arobaini (Tsh. 440,000,000) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa 22 katika shule nane (8) za sekondari.

| NA | JINA LA SHULE | IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|---|
| 1 | SHANGANI | 4 | 80,000,000 |
| 2 | BANDARI | 4 | 80,000,000 |
| 3 | CHUNO | 4 | 80,000,000 |
| 4 | MITENGO | 2 | 40,000,000 |
| 5 | NALIENDELE | 2 | 40,000,000 |
| 6 | SINO TZ | 2 | 40,000,000 |
| 7 | MANGAMBA | 2 | 40,000,000 |
| 8 | MTWARA TECH. | 2 | 40,000,000 |
| **JUMLA** | | **22** | **440,000,000** |

***Taarifa ilipokelewa na kukubaliwa***

**MUHT. NA. 149/2021: TAARIFA YA UONGOZI MWEZI OKTOBA 2021**

Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala aliwasilisha taarifa ya Utendaji kazi kwa mwezi Oktoba 2021.

Taarifa za Watumishi

- Idadi ya Watumishi
  - Mahitaji 1,811
  - Waliopo 1,294
  - Upungufu 517
- Ngazi ya Halmashauri vimefanyika vikao 12
- Ngazi ya Idara vimefanyika vikao 15
- Watumishi 89 walipewa ruhusa
- Watumishi 40 walipewa likizo
- Watumishi 36 wapo kwenye mafunzo ya muda mrefu
- Hakuna mtumishi aliyestaafu
- Hakuna mtumishi alieacha kazi

Watumishi 02 wamehama

| NA | JINA | IDARA | CHEO | ALIKOHAMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ally A. Ndale | Elimu Msingi | Mwalimu | Tamisemi-Dodoma |
| 2 | Daudi Mrutu | Elimu Sekondari | Mwalimu | Halmashauri ya Jiji la Dar-es-salaam |

Mjumbe alitaka kufahamu mshahara binafsi unakuwaje.

Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala alikieleza kikao kuwa mshahara binafsi ni mshahara anaolipwa mtumishi tofauti na cheo anachokihudumu kwa sasa, (kwa maana ya kwamba cheo alichonacho sasa kina mshahara mkubwa kuliko cheo anachopandishwa), hivyo bila kumuombea mshahara binafsi cheo kipya kitashusha mshahara wake.

Mjumbe alishauri Halmashauri itumie fursa ya kuwepo kwa chuo cha Afya na chuo cha Utumishi wa Umma ili kupunguza uhaba wa watumishi wa afya pamoja na watendaji wa mitaa kwa kuwaomba wafanye kazi za kujitolea.

Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala alikieleza kikao kuwa ni vigumu kuwatumia wanachuo kwa kuwa kada ya Afya inahitaji watumishi waliokamilisha taratibu za kitaaluma, hivyo wanafunzi wote wa vyuo hawawezi kutumika kwa kuwa hawajafuzu mafunzo.

***Taarifa ilipokelewa na kukubaliwa***

**MUHT. NA. 150/2021: TAARIFA YA MWENENDO WA KESI MWEZI OKTOBA 2021**

Mkuu wa Kitengo cha Sheria aliwasilisha taarifa ya mwenendo wa kesi kwa Mwezi Oktoba 2021.

| NA | PANDE BISHANI | MADAI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Makarani Mzee Shaweji na Wengine 193 dhidi ya<br>1) Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa<br>2) Mwanasheria Mkuu wa Serikali<br>3) Mkurugenzi wa Manispaa. | Madai ya maeneo yao ya Mbae, Kiholo, Califonia, Soko mjinga na Mangamba ambayo wana nyaraka za umiliki hivyo Mahakama itamke kuwa walalamikaji ndio wamiliki halali. | Kusikilizwa Tarehe 19/10/2021 |
| 2 | Peter A. Mohamed & Lucas Bununge na wengine dhidi ya Mkurugenzi wa Manispaa | Kuilalamikia Halmashauri kwa kushiriki kuhamisha umiliki wa Kiwanja Na. 115 Kitalu 'J' Kiyangu kutoka kwa mmiliki halali bila kufuata sheria | Shauri kusikilizwa 11/11/2021 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Hamisi Mohamed Bandari & Fatuma Ally Issa dhidi ya Mkurugenzi wa Manispaa na wengine (7) | Madai ya kurudishiwa / Kulipwa gharama za kesi | Tarehe ya uamuzi itatolewa na Mahakama kwa njia ya samansi |
| 4 | Omary Zuberi na wenzake 576 (TALGWU) dhidi ya Mkurugenzi wa Manispaa na mwingine mmoja | Maombi ya kuongezwa muda wa kukata rufaa | haijapangiwa |

***Taarifa ilipokelewa na kukubaliwa***

**MUHT. NA. 151/2021: MAOMBI YA AJIRA YA MKATABA KWA WATAALAMU WA KADA YA MAABARA**

Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala aliwasilisha taarifa ya ajira ya mkataba kwa wataalamu wa kada ya Maabara. Alikieleza kikao kuwa Ofisi ya Mkurugenzi imepokea barua ya tarehe 25/10/2021 ikihusu taarifa ya maombi ya ajira hiyo toka idara ya Afya ambapo nafasi zinazoombewa ni:

1) Mteknolojia Maabara daraja la II
   Ngazi ya mshahara TGHS B (Tsh. 680,000)

2) Mteknolojia Msaidizi Maabara
   Ngazi ya mshahara TGHS A (Tsh. 432,000)

Malipo ya mishahara kwa watumishi hawa wa mkataba yanapendekezwa yalipwe na kituo cha Afya Likombe kupitia mapato yao ya ndani. Pamoja na kuwasilisha ombi hili la ajira ya mkataba, ofisi ya Mkurugenzi inaendelea kufanya ufuatiliaji TAMISEMI ili kupata wataalamu watakaoziba pengo hilo kwa njia ya ajira ya kudumu.

Hivyo kwa kuzingatia taratibu za ajira ya mkataba ya dharula ofisi inapendekeza ajira hizi zitolewe kwa muda wa miezi mitatu mitatu ili kupima uwezo na ufanisi wa kazi za wataalamu hao.

***Wajumbe waliridhia ajira ya mkataba kwa Mteknolojia Maabara na Mteknolojia Msaidizi Maabara***

**MUHT. NA. 152/2021: TAARIFA YA USIMAMIZI WA SWIMMING POOL MASHUJAA**

Mkuu wa Kitengo cha manunuzi aliwasilisha taarifa ambayo inatoka kwa Mzabuni (Open Sanit Company Limited) wa S.L.P 70293 Dar es salaam yenye Kumb. Na. OGC.HQ/21/10 ya tarehe 20/10/2021 iliyopokelewa na Ofisi ya Mkurugenzi tarehe 25/10/2021 aliyepewa

zabuni ya kuendesha huduma ya mabwawa ya kuogelea (swimming pool) katika eneo la viwanja vya mashujaa kata ya Rahaleo.

Mzabuni alitakiwa asaini mkataba tarehe 22/09/2021 kama inavyoonesha kwenye barua yake ya kukubali kotesheni na kuanza kazi tarehe 01/10/2021 hadi tarehe 01/10/2022. Kabla hajasaini mkataba ameleta maombi yake ya kuongezewa maeneo ya usimamizi kama yafuatavyo: -

i. Kuongezewa eneo la uwanja wa mpira ili aweze kuweka michezo ya watoto na eneo la kuchezea.
ii. Vyumba vya kubadilishia nguo havina mahitaji ya watoto, hivyo wanahitaji kuongezewa
iii. Kuboresha eneo la uzio kuzunguka mabwawa
iv. Kuboresha eneo zima kimazingira (Landscaping)
v. Kuongezewa kipindi cha mkataba kutoka mwaka mmoja kiwe miaka mitano
vi. Kuboresha eneo husika kufikia viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa

Mjumbe alitaka kufahamu katika mkataba wa mzabuni endapo atashindwa njiani hataleta shida.

Mkuu wa kitengo cha manunuzi alikieleza kikao kuwa kwa uzoefu alionao mzabuni huyo hawezi kushindwa njiani.

Mjumbe alitaka kufahamu endapo mzabuni katika mkataba wake ataleta athari Halmashauri itaweza sitisha mkataba wake.

Katibu alikieleza kikao kuwa mkataba unakuwa na kipengele cha kusitisha mkataba

Mjumbe alitaka kufahamu kuwa endapo mzabuni ataboresha eneo haitaathiri mikataba ya wazabuni waliopo.

Katibu alikieleza kikao kuwa maeneo mengine hayataathiriwa.

Mjumbe alishauri mzabuni kupunguziwa muda wa mkataba wake kutoka miaka mitano (5) anayoomba kuongezewa na kupewa mkataba wa miaka mitatu (3).

Mjumbe alitaka kufahamu kama tozo itabaki ile ile ya mwanzo yaani Tshs. 300,000/= au michezo ya Watoto italipiwa.

Katibu alikieleza kikao kuwa kwa vile gharama za marekebisho zote ni zake, tozo inabaki Tsh. 300,000.

Mjumbe alitaka kufahamu kama mwekezaji atakapoondoka michezo ya watoto ataiacha.

Afisa biashara alikieleza kikao kuwa ataondoka navyo.

***Wajumbe waliridhia maombi ya mzabuni kwa mkataba wa miaka mitatu (3).***

**MUHT. NA. 153/2021: UTEUZI WA MWENYEKITI WA BODI YA ZABUNI**

Katibu aliwasilisha taarifa ya uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni kuwa amemteua Tamko Mohamed Ally (Afisa Utumishi na Utawala), uteuzi huu umefanyika baada ya kukamilika kwa kipindi cha miaka mitatu ya uteuzi wake wa awali wa Mwenyekiti wa Bodi aliyeteuliwa tarehe 30/11/2018, hivyo kufika tarehe 30/11/2021 kipindi chake cha uteuzi wa miaka mitatu kinafikia ukomo. Sanjari na kifungu cha 7(2) (a) cha kanuni za Mamlaka za Zabuni za Serikali za Mitaa za mwaka 2018 kimeelekeza kuwa Mwenyekiti anatakiwa awe ni miongoni mwa wakuu wa Idara kwenye Halmashauri.

Mjumbe alitaka kufahamu kama nafasi hii ya Mwenyekiti wa Bodi ni nafasi ya kuteuliwa au kuomba.

Katibu alikieleza kikao kuwa Mwenyekiti wa Bodi anateuliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mjumbe alitaka kufahamu endapo kamati haijaridhia uteuzi uliofanyika kamati ina nafasi ya kumkataa.

Katibu alikieleza kikao kuwa kama kuna sababu za msingi za kumkataa wanaweza kukataa.

***Wajumbe walikubaliana na uteuzi wa ndugu Tamko M. Ally kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni.***

**MUHT. NA. 154/2021 MENGINEYO**

a) Taa za Barabarani

Mjumbe alitaka kufahamu Halmashauri imejipangaje kuhusu taa za barabarani ambazo kwa sasa haziwaki.

Katibu alikieleza kikao kuwa dokezo limeandaliwa kwa taa za barabara ya Bandarini na Barabara kuu ya Mkoani pia barabara ya Chuno zitabadilishwa kwa awamu kwa kuwa Halmashauri ina changamoto ya mapato.

b) Mifereji ya maji

Mjumbe alikieleza kikao kuwa tunaelekea kipindi cha mvua, Kata ya Magomeni mifereji ilichimbwa nusu hivyo alishauri maeneo haya yaangaliwe mapema ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza.

Katibu alikieleza kikao kuwa wananchi wanajukumu la kushiriki kuchangia na nguvu kazi ili kuipunguzia Halmashauri mzigo.

Mkuu wa kitengo cha mazingira alishauri kuwa waonane na wadau ili waweze kuchangia gharama za mafuta.

Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala alikieleza kikao kuwa apelekwe mtaalamu ili kufanya makadirio ya mafuta yatakayotumika kwa kuwa inaweza tajwa gharama kubwa lakini uhalisia ikawa ni gharama ndogo.

c) Fedha za Upimaji

Mjumbe alikieleza kikao kuwa Halmashauri imetajwa kupokea fedha za upimaji hivyo alitaka kufahamu ni kwa sababu gani taarifa hiyo haijawasilishwa.

Katibu alikieleza kikao kuwa upimaji viwanja eneo la Mkangala Halmashauri imesaini mkataba wa fedha hizo ingawa mpaka sasa fedha hizo hazijaingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri.

d) Bwawa la Samaki

Mjumbe alitaka kufahamu mabwawa ya samaki yanayochimbwa Mtawanya, anaefanya shughuli za uchimbaji ni nani, msimamizi ni nani na fedha inayotumika ni kiasi gani.

Katibu alikieleza kikao kuwa suala hili linashughulikiwa ngazi ya Mkoa. Washauri wa mradi ni FETA waliopo Milumba Tarafa ya Mikindani, Halmashauri ilikua na jukumu la kutafuta eneo na kulisawazisha na kuwezesha upatikanaji wa miundombinu ya maji na umeme.

e) Fedha za Ujenzi wa Zahanati

Mjumbe alishauri kuwa fedha zote zinazoingia Halmashauri ziainishwe ili kama kupangiwa miradi zipangiwe na taarifa za fedha zitolewe kwa ufasaha.

Katibu alikieleza kikao kuwa Zahanati ya Ufukoni imepokea Tsh. 250,000,000 kwa ajili ya kujenga jengo la wagonjwa wa nje (OPD), Kichomea taka na Maabara. Mzabuni wa OPD na kichomea taka amepatikana lakini mzabuni wa maabara mchakato unarudiwa kwa kutangazwa upya nafasi hiyo ndani ya siku tatu.

**MUHT. NA. 155/2021 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 06:28 mchana.

| ..................... | **UMETHIBITISHWA NA:** | ..................... |
|---|---|---|
| **KATIBU** | 17/12/2021 | **MWENYEKITI** |
| | **TAREHE** | |